

# UQAB
Jarida la

Toleo 21 - Muharram 1440 H / Oktoba 2018 Miladi


**Afrika Inahitaji Mfumo Mbadala**

**Ufisadi ni Saratani Sugu ya Urasilimali**

**Safu ya Mbele ya Ulinzi kwa Ummah**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 17**

**SWALI/JAWABU: Mradi Mpya Juu ya Syria**





## Muharram 1440 Hijria Imewasili Lakini Waislamu Bado Hatuna KHILAFAH

# Muharram 1440 Hijria Imewasili Lakini Waislamu Bado Hatuna KHILAFAH




Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu Waislamu waliadhimisha Mwaka Mpya wa Kiislamu wa 1440H. Kwa kila Muislamu anayefuatilia hali ya Ummah wa Kiislamu ndani ya taifa hili na nje atatamaushwa na hali ya vile Uislamu na Waislamu wanavyodhalilishwa kila upande. Mfano hapa nchini Kenya Vita dhidi ya Ugaidi na Misimamo Mikali vimepelekea Waislamu wangapi kuuawa na kupotezwa na Uislamu kudhihakiwa na matukufu yao kuchafuliwa? Nchi jirani za Tanzania na Uganda ni Waislamu wangapi wanaosugua jela kwa tuhuma za Ugaidi? Afrika ya Kati (CAR) ni Maelfu ya Waislamu wangapi waliuawa? Tukija katika ardhi za Mashariki ya Kati namna zinavyoendeshwa na Vibaraka makhaini waliouza roho zao kwa wakoloni wa magharibi dhidi ya ndugu zao Waislamu watukufu; na badala yake kuzifanya Washington na London kama kibla chao. Huku Qibla cha Kwanza cha Waislamu Al Quds kikichafuliwa na umbile la kiyahudi kwa ushirikiano wake na ruwaibidha (Watawala duni) Tukiangalia Asia ya Kati (Tajikistan, Uzbekistan, Kyrgyzstan, Pakistan n.k) tunashuhudia maelfu ya Waislamu wakiozea magerezani kwa tuhuma za kutaka kujifunga na Uislamu Kikamilifu. Hivi sasa ndugu zetu wa Rohingya, Uiyghur, Syria, Crimea, Afghanistan, Libya, Kashmir, n.k wanaishi kwa mashambulizi ya kinyama ambayo nyuma yake yanaendeshwa na maadui wa Ummah huu mtukufu wa Kiislamu.

Masaibu haya yanayokumba Ummah yapaswa yamshughulishe kila Muislamu aliye na yakini na Siku ya Kiyama na kisha ajiulize ni mchango upi anaotoa ili kubadilisha hali hiyo? Na je mchango huo ana uhakika uko katika njia ya sawa kufikia hali ya mabadiliko yatakayopelekea Ummah huu kunusurika na majanga na uadui wa kitaifa na kimataifa?

Matatizo haya kwa hakika ni natija ya kuvunjwa kwa Khilafah (Utawala Wa Kiislamu) ambayo wanavyuoni wameitaja kuwa ndio mama na taji la faradhi zote. Dola ya Khilafah ilivunjwa na Uingereza ikishirikiana na Ufaransa na baadhi ya vibaraka ndani ya Ummah wa Kiislamu mnamo 28 Rajab 1342H sawia na 3 Machi 1924. Hadi kuvunjwa kwa Khilafah, wamagharibi hao walifanya kazi ya kumezesha Waislamu fikra hatari na sumu kwenye mabongo yao kama vile utaifa, ukabila na uzalendo. Na hii ni baada ya kuiona Khilafah haishindiki kijeshi kwa karne kumi na tatu! Naam, Waislamu mwanzoni ilikuwa hawashindiki kivita kwa kuwa itikadi yao ilikuwa safi kwenye vifua vyao huku wakipigana Jihadi ili kuhifadhi damu

*Endelea Uk..3*



Email: info@uqab.or.ke

za watu na kuondosha kila kikwazo dhidi ya kueneza uadilifu wa Uislamu. Fikra ya Jihad ilikuwa imekitwa ndani ya mioyo madhubuti kutokana na uchajiMungu uliokuwa umeshamiri katika Serikali ya Kiislamu tangu wakati wa Mtume (saw) mpaka Khalifah wa mwisho Abdulmajid wa Pili. Hapo ndipo wakabuni mikakati ya kuivunja Khilafah Uthmani kwa kuanza kuipiga vita kifkra hususan baada ya Khilafah ya mwisho kuanza kudorora katika ufahamu wao uliosababishwa na kurudi nyuma katika instinbaati (uvuaji wa Hukm katika masuala/matukio mapya). Mfano kushindwa kutofautisha baina ya hadhara na madania ipi ya kuchukuliwa na ipi ni ya kuachwa. Ambalo ilipelekea kushindwa na namna ya kulipatiliza suala la Mapinduzi ya Viwanda yaliyoibuka Ulaya na matukio mengine yaliyohusiana na kama hayo na hivyo kupelekea mgawanyiko ndani ya Dola.

Baada ya kuivunja Dola yetu wakatuletea itikadi ya usekula (kutenganisha na dini na maisha) na kutuwekea mfumo wao batil wa urasilimali na nidhamu zake chafu kwa kipimo cha faida/hasara/madhara/maslahi. Na kuigawanya iliyokuwa Dola moja ya Khilafah na kuwa vijidola 54 huku vyengine vikiongozwa na wafalme, wengine maraisi n.k lakini wote wakiwa ni vibaraka watumwa wa wakoloni walioivunja Dola tukufu ya Kiislamu ya Al Khilafah. Tokea wakati huo Ummah huu umezama katika maumivu mazito ya kuvunjiwa Dola yake na kubakishwa yatima bila ngao ya utetezi na ndio maana leo hii tumekuwa duni thamani juu ya mgongo wa ardhi na huku kila mjinga na asiyekuwa na nguvu anatudharau na kutunyanyasa hata kufikia hatua kutuua mamilioni kwa visingizio vya kila aina!

Hivyo basi ni jukumu la kila Muislamu popote alipo kuchangamka na kuhakisha kuwa Waislamu wanarudi tena katika hali yao ya Kuishi kwa mujibu wa Uislamu. Nayo ni kupitia kufanyakazi usiku na mchana na kusimamisha tena Serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Hakika kurudi kwa Khilafah ni ahadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt):

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْوَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia Amani baada ya khofu yao.** (An-Noor: 55)

Na ni bishara kutoka kwa Mtume (saw):

**ثم تكون ملكاً جبريا، فتكون ما شاء الله أن تكون، ثم يرفعها إذا شاء أن يرفعها، ثم تكون خلافة على منهاج النبوة، ثم سكت**

“…Kisha kutakuwepo na utawala wa utenzaji nguv, utakuwepo kwa muda ambao Allah atataka uwepo kisha Allah atauondoa wakati anapotaka kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah katika njia ya Utume,” Kisha akanyamaza. (Ahmad)

Ndugu zenu **Hizb ut Tahrir** wanawaita mujiunge nao katika kulibeba jukumu hili zito ambalo limewapelekea baadhi na wengi kati yao kuozea katika magereza ya viongozi hawa ruwaibidha na wakoloni. Ikiwemo hivi majuzi kutekwa nyara na majasusi wa nchi ya Pakista kwa wanachama wa kike kwa majina “Romana Hussain – Alfajiri ya 30 Julai 2018” na “Dkt. Roshan na Mumewe – Alfajiri ya 13 Agosti 2018” na huku wengine wakiuwawa na kupotezwa kabisa wasijulikane walipo.

Kwa kufahamu kuwa ni ahadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na bishara kutoka kwa Mtume (saw) matukio hayo ya kuogofya hayajapelekea wabebaji da’wah kurudi nyuma au kukata tamaa mbele ya hawa vikaragosi ambao Allah (swt) anawapa muhula kisha atawapa adhabu ambayo haina mfano wake. Kuuliwa, Kudhuriwa, Kufungwa gerezani au Kufutwa kazi n.k yote hayo ni Sunnah katika da’wah na ni mipango ya Allah (swt) ikiwa amekupangia ikufike:

قُلْ لَنْ يُصِيبَنَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَانَا ۚ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

**“Sema: Halitusibu ila alilo tuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mola wetu Mlinzi. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu.” (**At-Tawba: 51)

Kwa hiyo tuchangamkeni ndugu zangu wakati ni huu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

**“Enyi mlio amini, muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume wake anapo kuiteni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa”** (Al-Anfaal: 24)

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama Katika Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Afrika Inahitaji Mfumo Mbadala Na Sio China Wala Marekani




Mnamo 3–4 Septemba, 2018 viongozi kadhaa wa Afrika walihudhuria Kongamano kubwa la Kimataifa la Ushirikiano baina ya China na Afrika huko Beijing, China. Hili ni Kongamano la tatu tangu kuasisiwa rasmi kwa makongamano ya aina hii baina ya China na Afrika yanayojulikana kuwa ni majukwaa ya kujadili ushirikiano baina ya China na Afrika / Forum on China-Africa Cooperation (FOCAC).

Kongamano la kwanza la aina hii lilifanyika Oktoba 2000 mjini Beijing likileta mjadala mpana wa pamoja baina ya China na mataifa ya Afrika katika kukuza uhusiano na ushirikiano zaidi katika nyanja za kiuchumi na kibiashara. Kongamano la pili lilifanyika Disemba 2015 nchini Afrika Kusini ambalo pia liliwakutanisha viongozi wa Afrika na China ambalo alishiriki Raisi wa China Xi Jinping ambaye aliahidi China kutoa kiasi cha US$60 billioni kuunga mkono jitihada za maendeleo ya Afrika.

Baadhi ya viongozi walioshiriki Kongamano la karibuni nchini China ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, pia maraisi ama viongozi wa juu kama mawaziri wakuu kutoka nchi za Nigeria, Tanzania, Uganda, Zimbabwe, Botswana, Zambia, Gambia, Malawi nk waliwakilisha. Tangu kufanyika Kongamano la mwanzo mahusiano baina ya Afrika na China yamekuwa na kuimarika kwa kiasi kikubwa kiasi cha viongozi wa juu zaidi 40 wa Afrika wamezuru nchini China.

Ushawishi wa China barani Afrika katika uchumi na biashara umekuwa katika kiwango cha hali ya juu, ikijihusisha kwenye miradi mikubwa ya miundombinu kama ujenzi wa reli, barabara kubwa, mikopo, biashara, misaada nk. Kibiashara, China imetanua sekta hiyo sana ikilinganishwa na miaka ya 1980, ambapo thamani ya biashara yake na Afrika kwa wakati huo ilikuwa ni $1 billioni, ikaongezeka katika 1999, kuwa US$6.5 billioni, na katika mwaka wa 2011, US$166.3 billioni, na bado kila siku inakuwa. Kwa ufupi, biashara baina ya Afrika na China imekuwa kwa karibu asilimia 30 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hali hiyo imeifanya China kuwa mshirika wa pili mkubwa kibiashara katika bara la Afrika baada ya Marekani. Aidha, China imezipita kibiashara hata nchi zilizokuwa na athari ambazo ziliwahi kuwa makoloni ndani ya Afrika kama Ufaransa, ambayo thamani ya biashara yake ndani ya Afrika ni US$47 billioni.

Kunakisiwa kuna makampuni 800 ya kichina barani Afrika yakijishughulisha na ujenzi wa miundombinu, masuala ya nishati, kuekeza katika biashara mbalimbali zikiwemo za benki, wakijishughulisha pia na kutoa mikopo ya masharti nafuu tofauti na mikopo ya madola ya magharibi. Tangu mwaka wa 2000, zaidi ya deni la $10bn linalodaiwa nchi za Afrika yaaminika limefutwa na China. Huku ndani ya Afrika kukiwa na karibu wachina milioni moja wakiishi na kufanya kazi.

Dori ya China barani Afrika imekuwa ni mada yenye mjadala

**_Endelea Uk..5_**

mzito kwa muda mrefu hususan kipindi cha miaka 18 iliyopita tangu kufanyika Kongamano la kwanza la ushirikiano (Forum on China-Africa Cooperation (FOCAC) mwaka wa 2000. Hapana shaka China inanyonya na ina ajenda pana na ya muda mrefu ya kuendelea kunyonya na kufaidika sana na rasilimali za Afrika, na kimsingi inazitegemea kwa kiasi kikubwa rasilimali hizo. Kwa mfano, thuluthi ya nishati yake ya mafuta inatoka Afrika hususan kutoka Nigeria na Angola. Nigeria inauza mafuta ghafi kwa China kwa kiasi cha $4.7 billioni kila mwaka. [New York Times] China ina mikataba ya muda mrefu na dola hizo (Nigeria na Angola) katika suala la nishati ya mafuta kiasi cha nchi hizo kuweza kuipatia China mafuta mengi hata kuliko Saudia Arabia. Pia, China ina hisa kubwa katika mafuta ya Sudan na Niger. Pia, China imewekeza katika nchi kadhaa katika sekta ya gesi asilia. Daima China inaufungamanisha uwekezaji wake na suala la misaada, mikopo nafuu, kupatiwa zabuni za ujenzi na biashara kubwa. China inapata madini ya phosphates kutoka Morocco, shaba na cobalt kutoka Kongo na Zambia, (bati) platinum na chuma kutoka Afrika Kusini, mbao kutoka Cameroon, pamba kutoka Misiri nk.

Zaidi ni kuwa China inawekeza katika miradi mikubwa ya miundombinu katika maeneo ya kimkakati ambayo itamsaidia katika kuvuna rasilimali. Kwa mfano, China imewekeza $500 millioni katika kuihuisha reli ya Tanzania na Zambia kutoka machimbo ya shaba ya Zambia hadi bandari ya Dar es Salaam. Kando na mafuta na madini, China pia inaimarisha masoko yake katika Bara la Afrika katika sekta ya kifedha, masuala ya mawasiliano, bidhaa za nguo, magari, vifaa na huduma za kimawasiliano nk. Katika upande wa kifedha na kimawasiliano, benki kubwa ya China ICBC inamiliki hisa ya asilimia 20 ya Benki ya Afrika Kusini ya South Africa's Standard Bank. Kimawasiliano, kampuni zao kubwa zaidi za teknolojia ya kimawasiliano na vifaa vya mawasiliano za Huawei Technologies na Peer ZTE Corp zimejizatiti vya kutosha ndani ya Afrika.

Kuna baadhi wanaona harakati za China katika Afrika kuwa ni tatizo kwa ustawi wa Afrika. Huu ndio pia mtazamo wa madola ya kimagharibi hususan Marekani na madola ya Ulaya pamoja na wanafikra wao. Madola hayo ambayo yamekuwa kwa muda mrefu yana maslahi makubwa kiuchumi, kisiasa na kijeshi ndani ya bara hili. Ukweli unabakia kuwa China inasukumwa na ubepari katika uvunaji huu wa rasilimali za Afrika, kwa kuwa ni dola la kibepari kivitendo, licha ya kubakia na lakabu ya ujamaa katika maandishi na baadhi ya vionjo vichache. Hata hivyo, utetezi wa madola ya magharibi kwa Afrika dhidi ya China sio wa nia safi, bali ni kwa msukumo wa uroho wao wa kutaka kupora rasilimali hizo peke yao.

Marekani ambayo kwa sasa hivi ina vita vikali vya kibiashara na China kimataifa kwa kuweka kodi kubwa ya asilimia 25 kwa bidhaa za dola US$34 billioni na bidhaa nyengine za China, na China kulipiza kisasi kwa bidhaa za kilimo za kimarekani, inasukumwa na khofu kubwa ya namna China ilivyoibuka juu kiuchumi, licha ya kuwa haina ushawishi wa kimfumo kimataifa. Msukumo wa Marekani umeathiriwa na mtazamo wa 'Muhafidhina Mambo leo" walipoibuka zama za Bush kuitahadharisha Marekani kuwa China ni tishio, 'sio mshirika' kama awali kama walivyodhani bali ni 'mshindani thabiti' dhidi ya Marekani.

Marekani ambayo imekuwa ndio kinara mkuu kiuchumi duniani tangu mwaka wa 1881, leo imeshindwa na China kibiashara, kwa kuwa China ni mshirika wa kibiashara wa madola 138 katika madola 200, kiasi cha kuifanya China kuwa mbele kibiashara kiulimwengu hata kuliko Marekani. Bila ya kutaja mradi mkubwa wa China wa kujenga barabara ndefu/ Belt and Road Initiative (OBOR) kupitia nchi mbalimbali ili kuziunganisha na China kibiashara. Kwa hivyo, imekuwa ni ada ya wanasiasa wa Marekani wanapozuru Afrika kuitahadharisha Afrika juu ya athari ya China. Itakumbukwa kwamba aliyekuwa Waziri wa Mambo ya nje wa Marekani Rex Tillerson alipofanya ziara yake katika baadhi ya nchi za Afrika mwanzoni mwa mwaka huu, alishutumu kwa matamshi makali harakati za kiuchumi na kibiashara za China barani Afrika. Tillerson alikosoa sera za China kuwa zinaelemea mataifa ya Afrika kuitegemea China, akiongeza kuwa uwekezaji wa kuimarisha miundo mbinu ndani ya Afrika unaongeza mzigo wa madeni kwa Afrika na hautoi nafasi za kutosha za ajira kwa Afrika. Aidha, Hillary Clinton nae alipozuru Zambia mwaka wa 2011 alionya Afrika kwamba China ni Koloni Mambo leo [David Smith, The Guardian, July 19, 2012]

Wakati mvutano baina ya Marekani na China ukipambamoto, rai ya umma kwa baadhi ya viongozi wa Afrika na baadhi ya wanafikra wanaiona China ni mkombozi kwa Afrika wa kuliinua bara hili kwa fursa katika miradi mbalimbali mikubwa ya kimaendeleo. Na hii imekuja kutokana na mwelekeo wa China wa kuwa na masharti nafuu kuliko madola ya magharibi na kutojikita katika kujihusisha na siasa za ndani za nchi za Afrika. Kwa ufupi, China imejifunza sura mbaya ambayo nchi za magharibi wamejijengea katika muamala wao na Afrika, hivyo China imeshika mwenendo kinyume nao. Na kimsingi China haikukhalifu msingi wa fikra ya kibepari ya kujiongezea kwa namna yoyote. Bali inachoonekana kutokipa nguvu ni kutojijengea himaya ya kimfumo na ushawishi wa kisiasa katika nchi nyengine. Na hili limekuwa ni jambo linalotokana na msingi wa tareekh ya dola ya China kwa muda mrefu.

Mvutano huu wa rasilimali za Afrika ulikuwa uliamshe bara hili kutoka katika usingizi mzito ulioligubika kwa makarne. Rasilimali za Afrika zilivunwa kwa wingi wakati wa ukoloni na utumwa, kisha mbinu ikabadilishwa zikavunwa wakiwa chini ya jina la 'uhuru' kwa kuwatumia watawala wakala chini ya chama kimoja, kisha baada ya wananchi kuwachoka na kugundua uovu wa watawala chini ya chama kimoja, rasilimali zinaendelea kuliwa chini ya mfumo wa vyama vingi. Sambamba na hilo, sasa China nayo imekuja na mbinu na mkakati wake wa kutojali hata hizo siasa, wanachojali ni rasilimali tu. Mvutano huu maana yake bado Afrika ina utajiri mkubwa na rasilimali nyingi kiasi kwamba kila siku madola yanabuni njia na kuvutana baina yao namna ya kuzinyonya bila ya Afrika kunufaika katika kiwango stahiki.

Afrika haihitaji China wala Marekani kwa kuwa hayo ni madola ya kibepari, bali inahitaji mfumo mwengine ambao una uadilifu na haki katika kuzisimamia rasilimali na kuwanufaisha raia jumla. Mfumo huo ni Uislamu pekee ambao Marekani na China inapambana nao kwa kuwakandamiza Waislamu ndani na kimataifa. Afrika inastahiki kushika mwelekeo wa kimfumo mbadala baada ya kuamiliana na madola ya magharibi, na sasa inaamiliana na China ambayo inafuata mfumo ule ule kijanja, ambao ndio mfumo wa Marekani, Uingereza na Ufaransa unaoungamiza ulimwengu bila ya huruma.

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Ufisadi ni Saratani Sugu ya Urasilimali

Punde tu baada ya kuchaguliwa kwa muhula wa mwisho, Raisi Uhuru Kenyatta alitangaza kuwa anaanzisha vita vipya–vita juu ya ufisadi. Mapema mwaka huu 2018, katika vile vinavyoitwa Vita juu ya Ufisadi ambapo tumeona vichwa vikizunguka huku ari ya pamoja dhidi ya kuumaliza ufisadi ikianza. Baada ya kipindi cha muda mrefu, maafisa kadhaa wa serikali wamefikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayo husiana na ufujaji wa mali ya umma. Tumeona pia majumba yaliyo jengwa katika ardhi kando ya mito yakibomolewa. Naibu wa Hakimu Mkuu Philomena Mwilu alikamatwa na kufikishwa mahakamani juu ya mashtaka ya ufisadi. Vita vya Raisi juu ya ufisadi ndio azma ya hivi karibuni katika kupambana na uovu huo unaopelekea thuluthi moja ya bajeti ya Kenya iliyo sawa na thamani ya $6 bilioni kupotea kutokana na ufisadi.

Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC) inachunguza zaidi ya ripoti 3000 zinazohusisha maafisa wa serikali na umma wote katika serikali ya kitaifa na za kaunti. Makamu Mwenyekiti wake Sophia Lepuchirit alisema kipaumbele kimepatiwa kesi zinazohusisha watu wakubwa na rasilimali kubwa za umma. Katika mwaka wa fedha uliopita, EACC ilitangaza kuwa imepiga hatua katika vita dhidi ya ufisadi kupitia kukamilisha faili 183 za ufisadi na makosa ya kiuchumi na kuzikabidhi Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma na ambazo 135 kati ya hizo ziliidhinishwa kwa ajili ya mashtaka na huku 14 kwa hatua za kiidara. Kinaya ni kuwa tume hiyo iliyopewa kazi ya kupigana na ufisadi mara nyingi imejikuta katika janga hilo hilo.

Ufisadi katika serikali ya Kenya ya baada ya ukoloni una historia inayopanuka na kuanzia enzi za serikali za KANU za Jomo Kenyatta na Daniel arap Moi hadi serikali ya PNU ya Mwai Kibaki. Kenya imekuwa na sheria hizi kwa muda mrefu za kupambana na wizi katika sekta ya umma, kandarasi ghushi na ufisadi, na kwa kusitisha, isipokuwa kwa tofauti chache, hakuna kiongozi aliyekuwa na hisia nzito za kutosha kutekeleza au kuishughulikia kadhia hii inavyostahili. Hongo nyingi zinazotolewa na wakaazi wa mijini nchini Kenya ni ndogo lakini hata kubwa zinachukuliwa–hongo zenye thamani ya zaidi ya Shilingi 50,000 (€600, US$700) ni asilimia 41 ya thamani ya hongo zote kwa jumla. Ufisadi pia uko kwa kiwango kikubwa huku kila moja ya serikali zilizotangulia ikikashifiwa kwa kuhusika kwake. Katika utafiti wa hivi karibuni Kenya imeorodheshwa kama nchi ya tatu fisadi zaidi duniani. Katika mojawapo ya mahojiano na gazeti la Kidachi Handelsblad, Hakimu Mkuu wa zamani Willy Mutunga alisema Kenya imekuwa uchumi wa majambazi ambapo ufisadi umepenya katika ngazi zote za jamii.

Ufisadi umeenea pakubwa nchini na haukuzivamia tu taasisi za umma bali pia za kibinafsi. Kupitia sakata kuu za ufisadi kama zile za Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) almaarufu kama ‘Chicken Scandal’, Anglo Leasing na Goldenberg na ya hivi karibuni ya Huduma ya Taifa kwa Vijana (NYS) na nyingi nyenginezo, mabilioni ya mali ya umma yameishia matumboni mwa wanasiasa. Tume na taasisi kadhaa zilizobuniwa kupigana na ufisadi zimefeli vibaya mno kutatua janga hili, badala ya kupambana na tatizo la ufisadi; zimeishia kuzama ndani ya ufisadi. Hili liko wazi wazi. Kwani tangu kuundwa na kubadilishwa majina ya tume na taasisi hizi, bado kadhia ya ufisadi inaendelea na kuenea kwa kasi mno.

Kwa kuwa Kenya imejifunga na mfumo wa Kimagharibi wa kirasilimali, si ajabu basi kusibiwa na uovu wa ufisadi. Mfumo ulioathiriwa na ulafi mkubwa wa ulimbikizaji mali kwa njia zozote na gharama zozote. Hili hulifanya tabaka la wanasiasa ndani ya serikali ya kirasilimali kuzama ndani ya wizi na ufisadi.

Tafiti za kila mara zinazofanywa ambazo hatimaye huja na matokeo ya kuorodhesha mataifa kwa viwango vikubwa vya ufisadi, hongo, umasikini nk., zote hazisaidii na hazina tiba yoyote ya kudhibiti janga hili. Matokeo hayo husaidia tu katika kutupa maalumati na takwimu chache huku ulimwengu mzima leo ukiwa unakabiliwa na migogoro isiyo idadi. Licha ya hayo, tafiti hizi kawaida hulenga kupunguza aibu na uovu wa Urasilimali ambao daima tumekuwa tukisema ndio tatizo pekee la maafa yote yanayoukumba ulimwengu.

Viongozi na wanasiasa wote wa kirasilimali kamwe hawatarajiwi kuung’oa ufisadi kwani uhalisia wa uongozi katika mfumo wa kirasilimali ni fursa ya ulimbikizaji na ufujaji wa mali ya umma. Ili kuziba uovu huu katili ni kule kudumu kwao kubuni tume za kupigana na ufisadi huku tume hizo hizo zikitumiwa kama hifadhi za wafisadi.

Ama kuhusu upigaji wao kelele nyingi kwa jina la kushutumu na kufichua ufisadi hiyo ni hadaa tu na kuziba macho raia na kuamsha hamasa za umma kwa manufaa yao kwa kujionyesha kana kwamba wanawajibika kisiasa na kuwaotesha vidole mahasimu wengine wa kisiasa kama wabaya huku wote wakiwa gora moja kunapokuja uporaji wa rasilimali za umma.

Kwa kuwa msingi wa tatizo hili ni mfumo mchafu wa kirasilimali, suluhisho la kweli na la kihakika liko katika kuachana na mfumo huu wa kikatili. Kuubadilisha kwa mfumo adilifu ambao si mwengine isipokuwa Uislamu. Ufuatao ni mukhtasari wa vipi mfumo wa Kiislamu unapambana vilivyo na janga la ufisadi kihakika. Uislamu unawalaani wote wanaojihusisha na hongo na ufisadi.

- Jukumu na wajibu wa kupigana na ufisadi liko kwa watu wote na sio watu fulani au tume fulani pekee.
- Katika Uislamu, uongozi ni amana ambayo walioaminiwa juu yake watakwenda kuhisabiwa Siku ya kiyama.
- Uislamu unawataka viongozi kuchukua hatua kali dhidi ya yeyote anayejihusisha na ufisadi bila ya kujali cheo chao katika jamii.

Kupitia hatua hizi, Uislamu kwa karne kumi na tatu ulipokuwa ukitawala nusu ya dunia, kesi za ufisadi zilikuwa nadra kama kulikuwa na yoyote. Vile vile lau Khilafah itasimamishwa tena, janga la ufisadi na maovu mengine yatang’olewa kwa mara nyengine tena.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Majeshi ya Waislamu Ndio Safu ya Mbele ya Ulinzi kwa Ummah



Kila taifa kubwa huwa na mipaka maalumu ambayo haipaswi kuvukwa. Kutokana na hili, mataifa makubwa, hususan mataifa ya kimfumo, huchunga nguvu yao ya kijeshi pamoja na mfumo wao. Mataifa makubwa huchukua hatua ambazo zitalinda, kupanua na kuhakisha mifumo yao inatawala na hutumia nguvu yao ya kijeshi kufikia hili. Hivyo basi dola wakati huo huo hutumia nguvu za kisiasa, kijeshi na kimfumo. Lakini, kwa kuja mfumo wa kirasilimali na kutafakari kwake mambo kupitia uwezekano wa kiakili, majadiliano juu ya mipaka hii maalumu ya dola na mataifa yamekuwa ndio njia ya kivitendo kukabiliana na matishio ya kindani na kinje. Hii ilianza kwa uadui juu ya matukufu, kukiuka kwao na kuendelea kuchafua heshima. Sasa, watu wanashuhudia ukiukaji huu wa matukufu na heshima katika runinga, kana kwamba wanatazama kipindi au filamu. Na mandhari hizi kamwe hazika sisimua jamii ya kimataifa au jamii maarufu kunyosha kidole, isipokuwa kwa kiwango tu kinacho hitajika kutia shinikizo juu yao, maji yanapozidi unga. Sio kuzusha kusema kuwa njia mpya ya Kimagharibi ya kutafakari kupitia uwezekano wa kiakili ni njia duni zaidi ya tafakari kwa wanadamu. Huuwa uwezo wa akili kuhukumu uhalisia na kuchukua hatua sahihi, imara, hususan katika wakati ambapo ni lazima kutenda kwa haraka na kwa kukatikiwa.

Ummah wa Kiislamu ndio taifa pekee katika historia lililoipa akili ya mwanadamu haki yake inayostahiki na kuheshimu matukufu ya mataifa, kiasi ya kuwa ulikuwa ni mfano wa kuigwa, katika historia ya kale na ya hivi sasa. Mifano ya historia hii ya Kiislamu iko mingi.

Mfano mmoja ni namna RasulAllah (saw) alivyo amiliana na Maquraysh juu ya Mkataba wa kusitisha mapigano wa Hudaybiyah, pindi Maquraysh walipokiuka mojawapo ya vipengee vya amani kwa kuwapa washirika wake Bani Bakr silaha na kuwasaidia kwa pesa na watu katika vita vyao dhidi ya washirika wa Mtume (saw), Bani Khuza'a. Mojawapo ya masharti ya Mkataba wa kusitisha vita wa Hudaybiyah ilikuwa makabila pambizoni mwa Makkah yalikuwa na uhuru wa kuchagua kujiunga katika mkataba kwa kuhifadhiwa ima na RasulAllah (saw) au Maquraysh. Bani Khuza'a walichagua kuingia katika mkataba wa RasulAllah (saw) na ahadi yake, na Bani Bakr wakachagua Maquraysh na ahadi yao. Kwa hivyo, habari ilienea kuwa watu katika Bani Bakr waliwashambulia Bani Khuza'a na Maquraysh wakawasaidia Bani Bakr. Kufuatia hilo, Amr ibn Salim Al Khuzaa, kiongozi wa Khuza'a, alikuja kwa RasulAllah (saw) kumuarifu kuhusu shambulizi la khiyana la Bani Bakr, kwa usaidizi wa Maquraysh, katika khiyana hiyo, iliyokiuka sharti la vipengee vya Mkataba wa kusitisha vita wa Hudaybiyah. Alikuja Madina na kusimama mbele ya Mtume wa Allah (saw) katika Masjid An-Nabawy na kumuomba msaada, akisema,

يا رب إني ناشد محمدا　　حلف أبينا وأبيه الأتلدا
هم بيتونا بالوَتير هُجَّدا　　وقتلونا ركعاً وسجدا

**"Ewe Mola, hakika mimi namuomba Muhammad**
**Kwa mkataba wa baba yetu na babake, unaokirimiwa**
**Wametushambulia kwa ghafla**
**Na wakatuuwa tukiwa katika rukuu na sujudi"**

Ukiukaji huu wa wazi wa mkataba wa kusitisha vita pamoja na RasulAllah (saw) wa Maquraysh, ulitosha kwa RasulAllah (saw), kama kiongozi wa kihakika wa jeshi pamoja na kiongozi wa kimfumo na wa kisiasa, kutoa jeshi la Waislamu. Zaidi ya hayo, utoaji huu jeshi sio tu wa kuwapa afueni Khuza'a na kuitisha "msamaha" kutokana na khiyana hiyo, bali ni kuvunja ngome za Maquraysh na kuifungua Makkah. Na hii ni wakati ambapo Makkah ilikuwa miongoni mwa makabila ya Kiarabu katika Bara Arabu mithili ya Washington ilivyo sasa.

*Endelea Uk..8*

Mfano mwengine unaoashiria kutolegeza msimamo kwa Waislamu inaposhambuliwa hadhi yao, ni tukio la Bani Qaynuqa’. Yahudi mmoja kutoka kabila la Bani Qaynuqa’ alifichua uchi wa mwanamke wa Kiislamu. Muislamu mmoja akamuona sokoni humo na kumuua kwa heshima ya mwanamke huyo mmoja wa Kiislamu. Kisha, Mayahudi wengi walikuwako sokoni humo, wakampa shahada kwa kumuua Muislamu huyo na mambo yakachacha. Pindi habari hizi zilipomfikia Mtume (saw), pasi na kusitasita aliamuru kutoka kwa majeshi. Hili halikuwa tu kwenda kukusanya pesa za umwagaji damu (diyah) ya Muislamu yule aliyeuliwa au kuitisha msamaha kwa ajili ya mwanamke yule aliyedhulumiwa, bali ilikuwa kulizingira kabila lile, baada ya yeye (saw) kuamuru kufurushwa kwao.

Ama kuhusu kesi ya Bani Quraydhah, ambapo hukmu ya Sa’ad ibn Muadh (ra) ilikuwa si nyengine isipokuwa ni hukmu iliyojengwa juu ya maadili ya Kiislamu, na ilikuwa sawia na utukufu wa damu ya Muislamu na heshima yake.

Alihukumu kuuliwa kwa wanaume wao na kuchukuliwa matekwa kwa wanawake na watoto wao. Hii haikuwa ni hukmu kutoka kwa mtu aliyekuwa na kisasi cha kale dhidi ya Mayahudi hawa. Hukmu yake ilikuwa sambamba na mafundisho msingi ya Uislamu mtukufu, kiasi ya kuwa Wahyi uliridhia hukmu hiyo, kwa Hadith ya Rasulullah (saw),

«لَقَدْ حَكَمْتَ فِيهِمْ بِحُكْمِ اللَّهِ مِنْ فَوْقِ سَبْعِ سَمَوَاتٍ»

**“Hakika umehukumu kwa hukmu ya Allah aliye juu Mbingu ya Saba.”**

Mifano mitukufu ya kulinda mipaka maalumu katika historia ya Waislamu iko mingi. Wakati huo, Ummah na majeshi yake walibeba misimamo imara iliyo hitaji vita dhidi vya mara kwa mara, kuanzia vita kwa walioritadi ili kuilinda Itikadi ya Kiislamu, hadi ufunguzi wa ardhi, mithili ya Ufunguzi wa Amouriah kutokana na mwito wa mmoja wa wanawake katika wafungwa wa kike wa Roma miongoni mwa Waislamu huru, na ufunguzi wa Sindh kwa sababu ya haramia mmoja aliyeivamia meli ya Waislamu katika bahari wazi na kadhalika. Lakini, huo ulikuwa wakati ambao Waislamu walikuwa na umbile la kisiasa na kiongozi wa umbile hilo alikuwa wa kisiasa, kijeshi na kimfumo. Kwa hivyo huu ulikuwa wakati ambao mfumo wa Kiislamu ulikuwa ndio muongozo wa Ummah huu na dola yake, na hukmu za kisheria za Kiislamu zilikuwa zikitekelezwa juu ya uhalisia, zilizoitisha kuwepo kwa misimamo imara.

Hakika, kukosekana kwa Uislamu katika usimamizi wa Ummah na ule wa Itikadi ya Kiislamu katika sera ya kijeshi ya majeshi ya Waislamu, pamoja na kubadilishwa kwa watawala waliobandikwa na Wamagharibi juu ya vichwa vya Waislamu kutawala kwa ukafiri na kwa utaifa na uzalendo, Waislamu na majeshi yao hawanyoshi kidole kulinda matukufu ya Waislamu. Hii ndio hali ilivyo Palestina, Kashmir, Syria na sasa Burma au nyuma ilivyo kuwa Bosnia-Herzegovina miongoni mwa kwengineko. Lau muda wote huu, Ummah ungekuwa na kiongozi kama Mtume (saw), au Khalifah kama Abu Bakr (ra), Umar (ra) na Mu’tasim (ra), kamwe hawangewakubalia Mayahudi, isipokuwa watawaliwe kwa Sheria ya Allah, kama ilivyo elezwa katika Hadith ya Mtume wa Allah (saw),

«تُقَاتِلُونَ الْيَهُودَ حَتَّى يَخْتَبِيَ أَحَدُهُمْ وَرَاءَ الْحَجَرِ فَيَقُولُ يَا عَبْدَ اللَّهِ هَذَا يَهُودِيٌّ وَرَائِي فَاقْتُلْهُ»

**“Mutawauwa (yaani Waislamu) Mayahudi hadi mmoja wao atajificha nyuma ya jiwe, jiwe hilo litasema (kwa kuwasaliti), ‘Ewe mja wa Allah Yahudi huyu hapa nyuma yangu; muuwe.’”**

Na kwa Mabudha kamwe hawangekubali chochote kwao isipokuwa hilo. Hawangekubali kutoka kwa Amerika, isipokuwa yale ambayo Mtume (saw) aliwakubalia Maquraysh wakati wa Ufunguzi wa Makkah.

Na hawangekubali kutoka kwa Warusi isipokuwa yale ambayo Sa’ad ibn Muadh aliyahukumu kwa kabila la Bani Quraydhah na Ufunguzi wa Moscow … na kukubali yoyote mengine yasokuwa haya yanapingwa na Uislamu kama aibu, fedheha na kuipa kipaumbele akili, ambayo yote haya yanagongana na Uislamu. Allah (swt) asema,

وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ

**“...Na izza iko kwa Allah, na kwa Mtume wake, na kwa waumini, lakini wanafiki hawajui.”** [Al-Munafiqun: 8]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Gazeti la Ar-Rayah – Toleo 198**
**Bilal Al-Muhajer – Pakistan**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 17: Kujitambulisha Mtume (saw) kwa Kabila la Banu Amir bin Swa’ Swa’h

Katika Halaqa hii tutaangalia kujitambulisha Mtume (saw) kwa kabila la Banu Amir bin Swa’ swa’h

Asema ibnu Is’haq: Alinihadithia ibnu Shihab Az-Zuhriy, kuwa Mtume (saw) aliwajia Bani Amir bin Swa’swa’h, akawalingania kwa Allah, akijitambulisha, akasema mtu miongoni mwao anayeitwa Bahira bin Firas: Wallahi lau mie nitamchukua huyu kijana wa kiquraysh ningewatafuna Waarabu kwa huyu kijana...!

Kisha akamwambia Mtume (saw): Je, waonaje ikiwa sisi tutakufuata juu ya jambo lako hili kisha Allah akakupa ushindi dhidi ya wanaokukhalifu, Je, Utawala utakuwa kwetu baada yako...?

Akasema Mtume (saw): “Utawala uko mikononi mwa Allah anauweka atakapo...! Yule mtu Akasema: Je, unakusudia shingo zetu zitiwe vyembe na Waarabu kwa kukuhami wewe, kisha Allah akikupa ushindi utawala uwe kwa wengine...!

Hatuna haja na mambo yako...! Wakamkatalia...!

Katika hiyo Hadith kumetumika neno (الأمر) “Al-amru” ambalo halina maana isiyokuwa utawala na madaraka, inamaanisha kuwa Mtume (saw) alikuwa anafanya bidii kuchukua uongozi kupitia AHLUL QUWWAH WAL MAN’AH (watu wenye nguvu na mamlaka).

Akaendelea Mtume (saw) anawalingania watu kila anapopata nafasi ya hilo, unapofika msimu wa Hijja na watu kukusanyika kutoka pembe za Jaziratul Arab na kuja Makka, Mtume (saw) huwafuata makabila na kuwalingania katika Uislamu, pasi na kujali kuwa haya makabila yataikubali Da’wah yake, ama wataikataa, ama watajibu vizuri...!

Na hakusubiri sana, mpaka bishara za ushindi zikaanza kudhihiri kutoka Madina.

**Itaendelea katika UQAB Toleo 22…In Shaa Allah.**

# SWALI/JAWABU:
# Mradi Mpya Juu ya Syria



**Swali**

Yaliyotokea mjini Daraa kutokana na serikali kuyavamia kwa haraka maeneo yaliyo hamwa kwa miaka, na kufuatiwa na Quneitra na kabla ya hapo Ghouta na kabla yake Aleppo na dada zake, na macho yote sasa yanaelekea Idlib, hii inaonesha kuwa yapo mambo ambayo yanastahili kufanyiwa utafiti na utambuzi. Na tumeona dori ya Amerika na njama zake na dori ya vyama vinavyoiunga mkono na njama zake na kuidhinisha kisiri kwa Dola wadhamini uzuiaji wa ongezeko la ghasia, mithili ya Uturuki, au kushiriki ndani yake kivitendo mithili ya Urusi. Ni yapi yaliyojiri au yanayojiri? Ni vipi nchi hizi zimeweza kuyaingilia mapinduzi ya Syria kwa njia hii? Ni dori gani zilizocheza? Na ni kipi kifuatacho?

**Jibu**

1. Baada ya kuzinduliwa kwake mnamo 2011 na tishio lake la kumng'oa Bashar, kibaraka wa Amerika, na kuenea kwa hamasa za Kiislamu, na tishio lake la kubadilisha sura ya eneo hilo kuwa ya Uislamu, mapinduzi ya Syria yalikuwa ni tukio la mabadiliko katika ncha mbili zenye umuhimu mkubwa sana; kwa ncha ya kwanza yaliangazia nguvu imara za kieneo zisizofuata Amerika wala Ulaya. Hivyo basi, kwa mara ya kwanza katika kiwango hiki kulikuwepo na nguvu ya kipekee iliyochipuza ndani ya Umma pasi na mamlaka ya makafiri juu yake. Kwa ncha ya pili, Amerika, Dola kuu nchini Syria na ulimwenguni, ilishindwa kuyakomesha. Ilikuwa mithili ya miujiza!
Syria haikuwa chini ya mzozo wa kimataifa. Lakini mzozo ni kati ya Amerika na wafuasi wake na vibaraka wake, upande mmoja, na watu wa Syria upande mwengine, Ulaya haina ushawishi wowote juu ya Syria, kama ilivyo nchini Yemen na Libya kwa mfano. Amerika inaidhibiti serikali hiyo, wafuasi wake na vibaraka wake. Mzozo huo ni kati ya Amerika, wafuasi wake na watu wa Syria wenye ikhlasi.

Lakini, mapinduzi ya Syria yameikosesha usingizi Amerika, hata Raisi Obama alitaja kuwa nywele zake ziligeuka mvi: "Nina imani sana kuwa kiasi kikubwa cha mvi zangu kimetokana na mikutano yangu ya Syria" alisema. (Ra'I Al Youm, 5/8/2016)

2. Amerika imechukua njia mbili tofauti kufikia lengo kubwa kabisa la Amerika katika eneo hilo, nalo ni, kuyamaliza mapinduzi ya Syria, na kuendeleza utawala wa kibaraka:

a. Njia ya kwanza: ni kutoa usaidizi wote wa kifedha na kijeshi kwa serikali hiyo jijini Damascus ili isiporomoke, ikiwemo kuisukuma Iran na wanamgambo wake kwenda Syria kupigana bega kwa bega na Bashar, na kisha kuisukuma Urusi kwa njia hiyo hiyo. Raisi wa Urusi, Putin, alitangaza kuingilia kati kwa Urusi nchini Syria mwishoni mwa Septemba 2015 punde tu baada ya mkutano wake na aliyekuwa Raisi wa Amerika Obama jijini New York. Amerika imepiga marufuku mashirika na taasisi zote za kimataifa kutokana na tuhuma zozote za kihakika kwa serikali ya Bashar licha ya uzito wa uhalifu wake uliofikia kutumia silaha za kemikali.

Ingawa iliitishia serikali hiyo endapo ingetumia silaha za

*Endelea Uk..11*

kemikali, lakini haikufuatilia vitisho vyake kwa kuhofia serikali hiyo. Na hili ndilo lililotokea: Pindi serikali hiyo ilipotumia silaha za kemikali mjini Ghouta mnamo 21/8/2013, Amerika ilituma manuari zake za kivita kushambulia serikali hiyo, lakini ikasita kufanya hivyo ili kutoathiri dhati ya serikali hiyo kwa mashambulizi haya! Na kuipelekea kuporomoka kabla ya kupatikana kwa kibaraka badali, kwa sababu haijamuona katika Muungano wa Kitaifa wa Syria, ambao umethibitisha uwezo wa kujaza pengo hilo, hususan kwa kuwa umejianika wazi kutokana na mahusiano yake na Amerika na vibaraka wake, hivyo basi ndio sababu Amerika imerudi nyuma, na kukataa kwake ni dalili wazi kwa kila mwenye macho kuona kuwa Amerika inataka kuihifadhi serikali hiyo, licha ya shambulizi la kinyama la kemikali la serikali hiyo… Licha ya hayo mapinduzi nchini Syria yangali imara na hata kuimarika uwanjani.

b. Njia ya pili, ambayo ndiyo ya hatari zaidi, ni kuyadhibiti (mapindizi hayo); Amerika ilitangaza kuwa iko pamoja na mapinduzi ya Syria, kwa kuyahadaa makundi ya wapiganaji kwa sababu haikuyapiga vita hadharani, lau wangekuwa na utambuzi wangejua kuwa inawatumia wengine kwa kazi hii! Tayari tushawahi kutaja hili katika toleo lililochapishwa mnamo 11/10/2015, linalosema: "… hili hapa ndilo janga; Amerika inajionesha kuwa pamoja na wanamapinduzi, na ni vigumu kuwapiga vita hadharani, na wamesababisha uharibifu kwa serikali, lakini badali ya Amerika bado haijapatikana. Hivyo basi imeanzisha mchezo mchafu hatari wa kuipa Urusi kazi hii, ya kuisaidia serikali hiyo hadharani na kupigana na wanamapinduzi hadharani, na vita vyake vimehalalishwa, na serikali hiyo ilikuwa tayari kuiita Urusi, kwa agizo kutoka kwa Amerika, na hili ndilo lililotokea … Urusi ilikubali dori hii chafu na ovu nchini Syria ili kuihudumia Amerika!"

Hivyo basi Amerika ilisema kuwa inausaidia upinzani kwa pesa na silaha, lakini yalikuwa ni maneno matupu bila ya vitendo! Kwa sababu Amerika inazuia kuwasili kwa silaha zozote zenye athari kwa mapinduzi hayo kupitia Uturuki au Jordan, na ilituma baadhi tu ya usaidizi kama makoti ya kuzuia risasi pekee ili kumakinisha ile dhana kuwa imesimama pamoja na mapinduzi hayo. Na ilitangaza kusaidia na kutoa mafunzo, yaliyonufaisha watu wachache pekee, na wakati mwengine wasiozidi watano. Lengo la hili lilikuwa ni kuyavutia makundi hayo kwake. Amerika ilitarajia kuwa madai haya yangefichuka wakati wowote, hivyo basi ilitumia wafuasi wake katika eneo hilo, hususan Uturuki na Saudi Arabia katika enzi ya Mfalme Salman, mwanzoni mwa 2015, nchi hizi zilipewa kazi ya kuyadhibiti mapinduzi hayo, na kupata utiifu kutoka kwa viongozi wa makundi hayo na kuyayusha kitambulisho cha Uislamu katika mapinduzi hayo, na nchi mbili hizi zikatumia vyombo vyao vya ujasusi kufikia hili. Pamoja na ufadhili mchafu wa kifedha, mashekhe (walinganizi) waovu, na kutoa nafasi, hifadhi, jukwaa la vyombo vya habari, na pesa zenye sumu.

3. Kwa sababu mapinduzi hayo nchini Syria wakati huo yalikuwa imara katika malengo yake na Uislamu, ilikuwa ni muhimu kuongeza zaidi matumizi ya vyombo hivi vya ushawishi wa Amerika, baadhi ya duru hata pia zimeripoti kuwa baadhi ya makundi nchini Syria yalipokea karibu dolari bilioni moja! Kupitia usaidizi wa kifedha,na kupewa jukwaa la vyombo vya habari na umuhimu wake, na hifadhi na uzito wake, wafuasi wa Amerika "Saudia na Uturuki" ziliweza kupata ushawishi juu ya upinzani na makundi ya kijeshi, na zikayaunganisha na ujasusi wa nchi hizo, mpaka kila moja ya nchi hizo mbili, hususan kupitia nukta za kifedha na nguvu ya vyombo vya habari, ziliweza kuwaangazia viongozi wake na kunyanyua vyeo vyao, na kuyadhibiti makundi hayo kupitia wao! Amerika, kwa kutumia vibaraka wake wote na vyombo vyake eneo hilo, inataka kuyapotoa mapinduzi ya Syria na kuyakoroga malengo yake.

Ilitangaza kuwa lengo lake nchini Syria na katika muungano wa kimataifa ni kupigana na 'ugaidi' yaani kupigana na makundi ya mapinduzi ya Syria. Licha ya kujiingiza kwake katika vita nchini Syria tangu 2014, mashambulizi yake ya mabomu yalifungika kwa kuyashambulia makundi inayoyaita 'ya kigaidi'. Kamwe haishambulii majeshi ya Bashar, na inashirikiana na Urusi. Lakini, viongozi wengi wa makundi ya wanamgambo wanaiamini (Amerika) na kushirikiana katika oparesheni zao pamoja na vyombo vya ujasusi, MOM na MOC, na hata kujihusisha na vita inavyoviita "vita dhidi ya ugaidi", hivyo basi kuanzisha mapigano ya kindani na umwagaji damu haramu. Hili liliyakanganya mapinduzi ya Syria, ambayo yalianza kupigana kwa sura mbili, sura ya Amerika dhidi ya "ugaidi", iliyoongezwa ile sura asili ya "kuing'oa serikali hiyo". Makundi hayo ya wapiganaji yalikuwa chini ya shinikizo kutoka Uturuki na Saudi Arabia juu ya shinikizo zaidi la kimataifa la kuendelea zaidi na kujihusisha na sura ya Amerika, na kuyaondoa kutoka katika sura asili!

Kuingilia kati kwa Uturuki, "Ngao ya Furat" kulikuwa ndio hatima ya muondoko huo. Uturuki iliyataka makundi yake kujiondoa kutoka katika vita vya Aleppo na kuelekea kaskazini kupigana na ISIS. Hivyo basi, majeshi ya Bashar na washirika wake, Urusi na Iran yakafaulu kuukalia mji wa Aleppo mwishoni mwa 2016, katika oparesheni iliyofanana na Uturuki kuikabidhi Aleppo kwa Warusi na kisha kwa serikali! Majibu ya makundi ya kisilaha ya Uturuki na kujiondoa kwao katika vita vya Aleppo na kujihusisha kwao na sura ya Amerika dhidi ya "ugaidi" ilikuwa ni dalili hatari mno, kwani ilionyesha wazi wazi kuwa uongozi wa makundi hayo ulikuwa ukilishwa mamilioni ya dolari, na kuwa na ushawishi mkubwa juu ya makundi yao. Na kwamba iliiwezesha Amerika, baada ya kusubiri kwa muda mrefu, kufungua ukurasa wa matumaini ya kuyamaliza mapinduzi hayo ya Syria.

Sera ya Amerika iliendelea kuuongoza uwanja wa Syria katika mwelekeo wa kuyamaliza mapinduzi hayo, lengo ambalo Amerika ililiona lawezekana baada ya kufaulu na wafuasi wake kuchukua utiifu wa viongozi wengi wa makundi ya kijeshi.

Kisha Erdogan akarudia mandhari ya "Ngao ya Furat", akavumbua "Tawi la Zaituni" ili kuirahisishia serikali kuingia Idlib. Pindi serikali ya Syria ilipoanza kuisongelea Idlib na kuizunguka kambi ya anga ya Al-Duhur, Erdogan alivisukuma vita kuelekea Afrin! Karibu wapiganaji elfu 25 wa upinzani walishiriki, na kiongozi wa kijeshi eneo la Failaq Ash-Sham, Yasser Abdul Rahim, akathibitisha kuwa takriban wanajeshi elfu 25 kutoka Jeshi Huru la Syria wanashiriki katika oparesheni ya kijeshi ya Uturuki mjini Afrin … (Russia Today: 23/1/2018), hili lilifanyika kwa utambuzi wa Amerika na ridhaa yake. Waziri wa Kigeni wa Uturuki Mouloud Gaoucheğlu alisema kuwa "alijadili juu ya mgogoro wa Syria na kadhia ya vitengo vya usalama mipakani pamoja na Waziri wa Ulinzi wa Amerika James Matiss mnamo Jumatatu jioni (15/1/2018) nchini Canada," (Anadolu Agency 17/1/2018). Haya yalithibitishwa na taarifa za Amerika, zinazoashiria kuwa Tawi la Zaituni na kadhia ya Afrin na harakati za jeshi la Uturuki zilifanywa kwa ridhaa kamili ya Amerika na kwa mawasiliano

Endelea Uk..12

ya Urusi na Amerika, na kutokana na taarifa hizi: "Kitengo Kikuu cha Utoaji Amri za Kijeshi cha Amerika kilisema kuwa Uturuki iliwadokeza juu ya oparesheni ya kijeshi katika mji wa Syria wa Afrin." (Quds Press, 21/1/2018)

4. Mpangilio wa sera ya Amerika nchini Syria baada ya kusalimishwa kwa Aleppo ni kama ifuatavyo:

a. Kutuliza uwanja wa Syria: anwani kuu ya lengo hili ni mbinu ya Astana, ambapo Uturuki inayalazimisha makundi yanayoegemea upande wake, kujadiliana na Bashar, Iran na Urusi kusitisha vita. Mtindo huu ulimalizikia kwa yale yanayoitwa makubaliano ya "kupunguza joto la kivita", yaliyokuwa yanakwenda kutoka eneo moja hadi jengine.

Yalifika kusini, ambako mwanzoni makundi yake hayakushiriki katika majadiliano ya Astana, lakini hatimaye yakashiriki. Katika kipindi cha miaka miwili ya majadiliano hayo, Uturuki iliibuka kama mdhamini wa makubaliano hayo pamoja na Urusi na Iran. Nguvu za mapinduzi hayo za miaka yake ya mwanzoni zilizuia kusitisha vita kwa aina yoyote. Lilikuwa ni lengo lisilofikika la utawala wa Obama, lakini lilianza kupatikana kufikia mwishoni mwa utawala huo mnamo 2016 na kisha utawala wa Trump ukawasili.

Kutuliza uwanja wa Syria kulimaanisha kuwa Amerika ilitoa mwanya wa majadiliano pasi na vitisho vya moja kwa moja vya kuiondoa serikali ya Bashar kijeshi, lakini kwa majadiliano yanayothibitisha uhalali wa serikali hiyo na hivyo basi hakuna lolote katika maamuzi yake lililoashiria kuondolewa kwa Bashar. Hii ni kwa sababu Amerika iliutumia Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama, inalolidhibiti, na kuwatuma wafuasi wake, wajumbe, weusi, kijani na weupe, kuanzia Kofi Annan hadi Lakhdar Brahimi mpaka de Mistura, na ikaweka makongamano ya Geneva kuuleta pamoja upinzani wa serikali hiyo, kuanzia Kongamano la Geneva 1 mnamo 30/6/2012, yote yakiwa ni kuitambua serikali hiyo na kuihifadhi. Vile vile makongamano yaliofanywa Vienna, Vienna 1 na 2 mnamo 2015. Mojawapo ya mambo muhimu katika makongamano yaliyofanywa jijini Vienna, Vienna 1 na 2 ni kuhifadhi sura ya kisekula ya dola ya Syria na taasisi zake. Uamuzi wa hivi karibuni zaidi wa kimataifa ni ule uamuzi uliofanywa na Amerika yenyewe mnamo 18/12/2015 na kukubaliwa kwa pamoja na Baraza hilo, ni uamuzi unaofupisha maamuzi yote na natija za makongamano ya Geneva na Vienna kuhusiana na Syria, na kuyafupisha kwa azimio moja, nambari 2254.

Uamuzi huu umekuwa ndio maregeleo ya hali ya kisiasa nchini Syria, na nchi zote zinalingania kutekelezwa kwake yakiwemo makundi ya kisilaha chini ya ushawishi wa nchi saidizi zinazolingania wito huo. Azimio hili halilinganii kuondolewa kwa Bashar! Thibitisho la ulinzi wa Amerika kwake yeye na serikali yake, hii ndio hali iliyokuwa hadi Aleppo ilipokabidhiwa, na kisha kuyalazimisha makundi ya kisilaha kutofungua mipaka kukawa hakuna budi, na kisha kuyashinikiza kufikia hilo na kujifunga na kusitisha vita kikamilifu, na kuiacha serikali pamoja na Urusi na Iran (wadhamini wengine wa kupunguza joto la mapigano) kuliteka eneo la wanamapinduzi hao, moja baada ya jengine. Mdhamini wa tatu, Uturuki haikutoa kidole juu ya ukiukaji huo! Serikali ililipua kwa mabomu eneo la Bonde la Barada, hata kabla wino wa makubaliano ya kwanza ya kupunguza joto la kivita mwanzoni mwa 2017 bado haujakauka, huku mdhamini huyu ikitazama wazi wazi! Lakini kujihusisha kwao kulifikia kuhusisha ujasusi wao, pindi serikali hiyo ilipochochea vita vya Ghouta mashariki, katika oparesheni za "kupambana na ugaidi" mjini Ghouta "msemaji wa raisi wa Uturuki Ibrahim Kalin katika mkutano wa waandishi habari mnamo Jumatano katika idhaa ya habari ya TRT alisema kuwa Uturuki haitaki uwepo wa mashirika ya misimamo mikali eneo la Ghouta mashariki." (Reuters, 15/3/2018) Alisema haya huku serikali hiyo, Urusi na Iran na wafuasi wao wakiilipua Ghouta kinyama kwa kwa mabomu, kana kwamba Erdogan wa Uturuki anahalalisha kitendo chao!

b. Kuhusisha sera ya Amerika kwa jina la "kupambana na ugaidi": Baada ya Raisi wa Amerika Trump kutangaza nia yake ya kuimaliza ISIS, na katika kupanua vita vya Mosul, Amerika ilifuata sera hii kwa sura nne:

- Sura ya kwanza: jeshi la Amerika liliyaongoza makundi ya Kikurdi, yanayosaidiwa na Amerika kuitoa ISIS kutoka Raqqa, na pia liliyaongoza makundi mengineyo eneo la mashariki mwa Syria kupigana na ISIS. Hivyo basi Wakurdi walikuwa na udhibiti mkubwa kaskazini mwa Syria, haswa katika maeneo ya Kikurdi nchini Syria. Nguvu kuu za Kikurdi zilikuwa ni Chama cha Kidemokrasia cha Kikurdi (KDP). Kwa usaidizi kutoka Amerika kiliweza kulimiliki tena eneo kubwa zaidi kutokana na udhibiti wa ISIS na kuyachukua maeneo yote ya mashariki mwa Furat; yaani asilimia 18 ya ardhi ya Syria, na ndio eneo lililo na utajiri mkubwa zaidi wa mafuta na gesi, pamoja na maji na rasilimali za ukulima, kuanzia Kobani hadi Raqqa, eneo la Bukamal na maeneo ya Deir al-Zour. Na hili halikuiathiri serikali hiyo. Majeshi ya Kikurdi huenda kwa mujibu wa maagizo kutoka kwa Amerika na hivyo basi hayakusimama usoni mwa serikali hiyo. Vyombo vingi vya habari hivi majuzi vilisambaza ripoti za kukabidhiwa maeneo kwa Vitengo vya Usalama vya Raia, kiungo kikubwa chenye nguvu za kidemokrasia ndani ya Syria, kutokana na maagizo ya Amerika, kwa serikali ya Syria; kwa msingi wa makubaliano yaliyofanyika jijini Damascus na Qamishli.

"Kiongozi wa Baraza la Kitaifa la Kikurdi nchini Syria, Fuad Aliko, alifichua sababu na mabadiliko yaliyokishajiisha Chama cha Kidemokrasia cha Muungano wa Kikurdi "PYD" kufanya makubaliano ya kisiri na serikali ya Syria, na serikali hiyo kupokea maeneo yaliyo chini ya udhibiti wa majeshi ya Kikurdi kwa msingi wa masharti na mambo yaliyo katika makubaliano hayo, ikiwemo mtaa wa An-Nashwa katika mji wa Hasaka, na maeneo mengine mashariki mwa Mto Furat." (https://arabi21.com, 16/07/2018) Na tovuti ya Herapolis (http://www.hierapolis.net) ilinukuu duru binafsi isiyo jina, kuwa mkutano ulifanywa Jumamosi iliyopita, "baina ya vinara wa wanamgambo wa KDP wanaowakilisha baraza lake la kijeshi la Munbaj, na maafisa wa serikali ya Assad katika makao makuu ya Chama cha Baath jijini Aleppo". Aliongeza kuwa walijadiliana "kulikabidhi eneo la usalama katika jiji la Manbaj kwa wanamgambo wa serikali pamoja na Bwawa la Mashahidi (Bwawa la Tishreen) kusini mashariki mwa jiji hilo." (www.qasioun-news.com, 11/07/2018)

Na viongozi hao wa makundi ya Kikurdi eneo la kaskazini mwa Syria wako chini ya udhibiti wa Amerika, ikiwa Amerika itawataka warudi katika mikono ya kibaraka wao Bashar, hawatakataa. Ipo ishara ya hili, gazeti la mtandaoni la "Ra'i Al-Youm", 7/6/2018 lilimnukuu kiongozi mkuu wa Wakurdi Salih Muslim akizungumzia kuhusu kukimbilia kujadiliana na serikali hiyo, alisema: "Milango yetu daima imekuwa wazi kwa kila mtu na tumeona tofauti katika mazungumzo ya Assad ya hivi karibuni. Haya ni maendeleo … na kama vile kila mtu anavyoyafikiria maslahi yake sisi pia tutafanya vivyo

***Endelea Uk..13***

hivyo". Taarifa ya Waziri wa Kigeni wa serikali ya Syria, Walid al-Muallem ilinukuliwa na gazeti la Al-Arab lililo na makao yake jijini London, 27/9/2017: "Wakurdi wa Syria wanataka muundo wa kujitawala wenyewe ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, na hii ndio kadhia ya majadiliano na mazungumzo". Serikali hiyo na Wakurdi ni karata za Amerika ambazo haziwasilishi vikwazo vyovyote kwa hali ya kisiasa. Kile Amerika inachotaka kwao wao hawakipingi wa serikali hiyo haikipingi, ima wabakie kama walivyokuwa, kabla ya 2011 au pamoja na utawala wao huru ndani ya Syria.

- Sura ya pili: iliongozwa na Uturuki katika vita vya Ngao ya Furat kaskazini mwa Aleppo mnamo 24/08/2016 na kisha Tawi la Zaituni mnamo 20/01/2018, iliirahisishia serikali kuingia Aleppo na kusini mwa Idlib. Ni kwa sababu makundi haya yaliagizwa na Uturuki na kuacha mapigano na serikali, na kujihusisha na kupigana katika ngao na tawi hilo, Aleppo na kusini mwa Idlib zilipotezwa au karibu na kupotezwa! Kabla ya hapo, Uturuki, ambayo inaendelea mpaka leo chini ya maelekezo kutoka kwa Amerika, katika kucheza dori nyengine mjini Idlib na kuingia eneo hilo kwa vikosi vya upelelezi kuanzia 7/10/2017 na kisha kupeleka majeshi yake na kuunda vituo vya uchunguzi ndani ya makubaliano ya kupunguza joto la kivita pamoja na Urusi na Iran … Baada ya hapo mkutano wa Erdogan pamoja na Raisi Trump ulifanyika mnamo 21/9/2017 jijini New York, Trump alimsifu Erdogan wakati huo kama: "rafiki yangu" (Anadolu, 21/9/2017) na mazungumzo baina yao yaliangazia hali nchini Syria. Trump alikubali Uturuki kuingia Idlib "jeshi la Uturuki limeanza oparesheni ya utafiti katika mkoa wa Syria wa Idlib kwa lengo la kubuni eneo la kupunguza uhasama chini ya makubaliano ya Astana. (Sky News Arabia 09/10/2017). Kwa mujibu wa tovuti ya 'Inab bakadi mnamo 13/5/2018, oparesheni ya Uturuki ingali inaendelea, ilisema: "Uturuki imekamilisha hatua zilizoanzishwa mkoani Idlib na inakwenda kwa mielekeo miwili wa kwanza ni utumizi wa vituo vya udhibiti vilivyo kuafikiwa katika makubaliano hayo ili kuhafifisha uhasama katika Astana, na mwengine ni uandaaji muundo wa kijeshi wa makundi yanayofanya kazi yasiyo kuwa na maelewano na makundi ya Kiislamu hadi leo …" Tovuti hiyo iliongeza pia: "Tangu mwanzoni mwa mwaka huu, vituo vya uchunguzi vya Uturuki vimetumiwa mjini Idlib katika mpaka ulio mashariki mwa Idlib kando na eneo la magharibi, ambayo imeibua maswali kuhusu sababu zilizopelekea kuviweka vituo hivyo upande wa mashariki pekee!" kwa mujibu wa duru, makundi hayo yalipokea usaidizi wa Uturuki mara moja pekee fv…

Licha ya hatua za Uturuki, mashambulizi ya anga ya Urusi yanaendelea, ambayo ndio kadhia chungu katika mandhari ya kila siku mjini Idlib. Kwa mujibu wa wanahabari wa 'Inab Baladi mjini Idlib na viunga vyake: "mashambulizi ya anga ya Urusi yanalenga eneo la kusini mwa Idlib kwa makombora yenye vilipuzi vikali mno yanayosikika kote Idlib."

- Ama kuhusu sura ya tatu, Amerika imeiingiza serikali ya Saudi, iliyo shiriki nayo katika muungano wa kimataifa, na kutangaza kwamba iko tayari kutuma majeshi yake ya ardhini hadi Syria kwa ajili ya Amerika na uongozi wake.

Serikali hii ilicheza dori chafu, kama serikali ya Uturuki, kupitia kuyaweka makundi ya kisilaha yaliyotiwa sumu na pesa zake chini ya ushawishi wake na kuyazuia makundi haya kutokana na kwenda katikati ya jiji kuu la Damascus, ingawa ilikuwa karibu na machoni mwao na umbali wa kurusha jiwe tu! Iliyoyafanya kukubali majadiliano na serikali, ikiyafanya makundi hayo kuanguka ndani ya ushawishi wake kupitia ufadhili wake kutoka Riyadh na kukubali kushiriki katika majadiliano hayo na hivyo ndivyo ulivyokuwa mkutano wa Riyadh 1 mnamo 11/12/2015. Taarifa ya Riyadh, na kongamano la Riyadh 2 ilitolewa mnamo 22-24/11/2017; na uliundwa ujumbe wa pamoja ili kujadili pamoja na serikali jijini Geneva na Vienna chini ya uongozi na mipango ya Amerika. Serikali ya Saudi ingali iko tayari kutoa huduma kwa Amerika. Mfalme mtarajiwa wa Saudi Bin Salman alisema baada ya kukutana na bwana zake nchini Amerika, akitangaza kile walicho muagiza kusema katika Jarida la Time mnamo 6/4/2018: "Siamini kuwa Bashar ataondoka bila ya vita, na siamini kuwa kuna yeyote anayetaka kuanzisha vita hivi."

- Sura ya nne ilikuwa ni majeshi ya Bashar, Iran na Urusi: baada ya kudhaminiwa na Uturuki "kupunguza joto la kivita" katika maeneo makuu, kama majeshi ya sura hii yalipigana vita mjini Palmyra na kufikia Deir al-Zour, yote kwa ushirikiano wa Uturuki na Saudi Arabia na ushawishi wao kwa makundi hayo, waliyapotosha mwelekeo makundi hayo kutokana na kupigana na katili hadi kupigana kwa sura nyengine chini ya kisingizio cha kupigana na 'ugaidi'. Hivyo basi serikali ikapata pumzi ya afueni na kujikukuta vumbi la kushindwa kwingi ilikokupata wakati wote wa mapinduzi.

Ilibuka yenye nguvu katika raundi zote za majadiliano jijini Geneva pamoja na Astana, ambapo ilikuwa ikizungumza kwa msimamo imara na kujiondoa kutoka katika majadiliano hayo. Makundi hayo yalianza kuziomba nchi kutia shinikizo kwa serikali hiyo kukubali suluhisho la amani, baada ya kuwa yalikuwa ni matakwa ya serikali hiyo kukomesha kuangamizwa kwake!

c. Kuziweka mbali sura zenye kuvuruga: pamoja na Amerika kuzitenga nchi za Ulaya kutokana na mandhari ya Syria, na kutaka kujibakisha wao na Urusi pekee kimataifa. Ingawa Urusi si umbile huru na Amerika nchini Syria, Amerika imeitumia Urusi kusimama na Bashar kama sura ya majadiliano ya kimataifa kuhusiana na Syria, ili kuzuia uingiliaji kati wa Ulaya. La muhimu pia, Amerika imetafuta kupunguza sura za kieneo zisije kutoka katika michoro, Qatar na Jordan.

Ama kuhusu Qatar, Amerika imezisukuma Saudi Arabia na Misri dhidi ya Qatar na kulazimisha kuisusia katikati mwa 2017 ikiituhumu kufadhili "ugaidi" nchini Syria, na kwa hivyo serikali hiyo nchini Qatar ilijipata chini ya tishio la moja kwa moja kutoka kwa vibaraka wa Amerika, hivyo basi ikakatiza kuingilia mambo nchini Syria, na kumaliza dori yake thabiti. Ama kuhusu Jordan, pamoja na ujasusi wake ilikuwa imeasisi mahusiano imara pamoja na makundi ya kusini mwa Syria, na hili lilikuwa kwa faida ya Uingereza kwa matarajio ya kupata baadhi ya ushawishi kwa Syria … Na kulidhibiti hili, Amerika imeanzisha hatua ya kibinafsi kufungua majadiliano pamoja na Urusi kwa ujanja wa "kupunguza joto la kivita" kusini mwa Syria, na hivyo basi ikaiwezesha serikali kuwa na takriban udhibiti kamili wa kusini na kisha kumaliza ushawishi wa kihakika wa Jordan au kukaribia kufanya hivyo.

Yaani, Amerika inakata matumaini yoyote ya ushirikiano wa makundi haya pamoja nayo ambao utayapa nguvu! Kama ilivyo nukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari, inaonekana kwamba baadhi yao yamezinduka kutokana na ujinga wao, na kusema kuwa Amerika imewahadaa! Sasa ndio wametambua?

5. Tunapoichunguza sera ya Amerika kwa makini na sera

Endelea Uk..14

ya wafuasi wake, hususan Uturuki na Saudi Arabia, na Misri kwa kiwango kichache kutokana na matatizo ya kindani, tunapata kuwa Amerika inakwenda kwa wakati huo huo katika mipangilio yote iliyochora kwa Syria na iliyotajwa juu, inauwacha mlango wazi kwa juhudi za serikali, Urusi na Iran kuushambulia upinzani kijeshi, na kuondoa matumaini yoyote ndani ya upinzani kuwa Amerika itasimama kuyasaidia.
Pindi serikali ilipoanzisha kampeni yake dhidi ya Daraa na eneo la kusini, likiungwa mkono na idara ya anga ya Urusi, Amerika ilituma ujumbe kwa makundi hayo ya Jeshi Huru kupitia ubalozi wake nchini Jordan mnamo 23/6/2018 ikisema: "Tunafahamu kuwa nyinyi ni lazima mufanye uamuzi wenu kwa mujibu wa maslahi yenu na maslahi ya familia zenu na kundi lenu kwa maono yenu, na hamupaswi kujenga uamuzi wenu juu ya dhana au matarajio ya sisi kuingilia kati kijeshi" ('Inab Baladi website, 23/6/2018). Na maana yake ni kuwa, Amerika inakata matumaini yoyote ya ushirikiano wa makundi haya pamoja nayo kwamba itasimama kuwaokoa! Kana kwamba baadhi yao, kama ilivyonukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari, wamezinduka kutokana na ujinga wao, na kusema kuwa Amerika imewahadaa! Sasa (ndio wamejua)?

Hivyo basi, Amerika inaifuata vilivyo sera ya kuyamaliza makundi ya kisilaha nchini Syria kupitia serikali, Iran na Urusi, na kwamba hayawi ni vikwazo vyovyote njiani, lakini mbele na nyuma ya hilo, ni mchango halisi wa Uturuki na Saudi Arabia! Usaidizi wa Amerika kwa makundi haya unakomea katika mipaka ya taarifa au pesa zilizolipwa kwa viongozi wake kwa mkabala wa utiifu. Kulikuwa na silaha chache zilizokuja kutoka Amerika na hazikuwa madhubuti kwa maumbile ya ulinzi (yaani hazikuwa za maangamivu), hilo lilifanyika wakati wa nyuma ili kuwakinaisha wanamapinduzi kuwa Amerika iko pamoja nao na inawaunga mkono ili wapate kuwa watiifu kwake. Leo, baada ya kuwa upande wa kijeshi wa Bashar Assad unashinda, mazungumzo yote haya yamemalizika, na taarifa za Amerika kuhusiana na hili zimekwisha; Amerika imefunga faili hili, vile vile wafuasi wake, Uturuki na Saudi Arabia.

6. Ama kuhusu mwelekeo wa majadiliano ya kisiasa, Amerika imekuwa ikiyaakhirisha hadi mapinduzi hayo yamalizwe na Bashar asimame tena kwa miguu yake. Hivyo basi, ilikuwa ikiwashughulisha wafuasi wake na vibaraka wake kutayarisha suluhisho kwa mazungumzo ya pembeni hadi hali za suluhisho la kisiasa zitakapokomaa na kuchukua wadhifa mkuu.

Hii ndio sababu wakati majadiliano ya kisiasa yalipokuwa yakiendelea yaliyochukua muda wa miaka miwili, vibaraka wa Amerika na wafuasi wao nchini Saudi Arabia na Uturuki walikuwa mbioni katika kupanga mikutano na makongamano ya upinzani wa Syria, na walikuwa wakiangazia viongozi katika mandhari ya kisiasa na kuwaondoa viongozi wengine. Yote haya yanafanyika hadi serikali hiyo itakaposimama tena kwa miguu yake, ndipo Amerika ichukue udhibiti juu ya hali ya kisiasa pamoja na dori ya Urusi au pasi na kuipa dori.
Lakini baada ya mafanikio makubwa ya kijeshi ya Bashar na washirika wake katika mji wa Aleppo, kisha bonde la Barada na Qalmon, kisha mashariki mwa Ghouta na kuondolewa kwa hatari kutoka pambizoni mwa jiji kuu la Damascus, na kisha katika vijiji vya Homs na Hama, na leo mjini Daraa, na pengine baadaye mjini Idlib na vijiji vyenginevyo vya Aleppo. Mafanikio haya makubwa yanaashiria kuwa suluhisho la kisiasa la Amerika linakaribia, lakini imeliakhirisha hadi baada ya Idlib. Inaonekana kana kwamba wanajitayarisha kwa hili, wamekamilisha utekelezaji wa makubaliano ya Fo'a na Zabadani; na makubaliano ya mwisho baina ya Urusi na Uturuki yaliidhinishwa mnamo 17/7/2018 na yanahusisha kuondolewa kwa wakaazi wa miji ya Fo'a na Kafriya walio watiifu kwa serikali katika mkoa wa Idlib waliozingirwa na makundi, ili makundi hayo yasimiliki karata yoyote ya shinikizo, na ili serikali isifedheheke ikiwa italishambulia eneo hilo na kutekeleza mauwaji. Hivyo basi, eneo pekee lililobakia bila ya suluhisho la kisiasa ni Idlib na pamoja nalo ni vijiji vya Aleppo, ambalo ni eneo muhimu lililo na mkusanyiko mkubwa wa wanamapinduzi, lakini Uturuki inaushawishi mkubwa juu ya mengi ya makundi ya kisilaha ndani yake, inatarajiwa kwa Uturuki kuyatia shinikizo kuzikabidhi silaha nzito kwa serikali hiyo na kufanya maridhiano nayo.

Hili ni hatari zaidi kuliko vita vya serikali, Urusi na Iran, ingawa yote ni hatari na yenye madhara … ikiwa nguvu ya kijeshi itaondolewa kutoka katika mapinduzi ya Syria, basi suluhisho la kisiasa la Amerika litakuwa chini ya matayarisho na utekelezaji … inatarajiwa zaidi kwamba Amerika inataka kumbakisha Bashar kwa muda wa "mpito" ambapo ni sehemu ya suluhisho lake la kisiasa, na kuhakikisha kipindi hicho cha umalizaji upinzani, na kisha kumleta kibaraka mithili ya Bashar atakaye endeleza kudumisha ushawishi wake nchini Syria, pamoja na kuweka usalama kwa binti yake umbile la Kiyahudi mvamizi wa Palestina. Umbile hili la Kiyahudi linataka kibaraka nchini Syria mithili ya Bashar ili kulinda usalama wake na asiyerusha hata risasi moja kwake. Netanyahu aliwaambia maripota kabla ya kuondoka Moscow mnamo Alhamisi 12/07/2018: "Sisi hatuna shida na serikali ya Assad (baba na mwana) kwa muda wote wa miaka arubaini, hakuna hata risasi moja iliyorushwa kutoka milima ya Golan. Hatupingi suluhisho la Raisi wa Syria Bashar Assad, bali tutafanya kazi juu ya kulinda mipaka yetu" (Ha'aretz, Julai 12, 2018)

7. Nguvu za kijeshi za serikali ya Syria ni dhaifu na zisizotosheleza kudhibiti Syria baada ya suluhisho la kisiasa. Jeshi la Bashar limezidi kuwa na uchovu. Licha ya kuendelea kusambaziwa silaha kutoka katika njia tofauti tofauti za Amerika, ima kupitia Urusi, Iran au kwengineko, nguvu kazi imebakia kuwa ndio tatizo lake kubwa. Hivyo basi, inatarajiwa kuwa suluhisho lolote la kisiasa la Amerika ni lazima lijengwe juu ya nguvu itakayolilinda. Amerika huenda akafuata moja ya njia mbili zifuatazo au zote, nazo ni:

a. Kuendelea kuitegemea Iran, chama chake na wanamgambo wake wengine, wakiwemo Wairani, Waafghani, Wapakistani nk., inayowajibisha kuwapa makao na uraia, ambapo baadhi ya habari zadokeza utekelezwaji wake leo na serikali ya Syria. Mjuzi mmoja alikisia katika shirika la habari la Ujerumani la DW, 30/4/2018, idadi ya wanamgambo hawa kuwa 45 na idadi ya chembe chembe zao kukaribia elfu 40, mjuzi huyo alisema: "Nadhani kuwa wanamgambo hawa watabakia nchini Syria … Tuliona mchakato wa kuwamakinisha katika ukanda wa Damascus. Wanamgambo wa Kishia wako katika kijiji cha Sayeda Zeinab na maeneo mengine … Nadhani kuwa Iran inajaribu, kama ilivyo hali kwa halaiki hiyo ya watu, kupewa kwao uraia au njia nyenginezo za kuwasaidia kubakia eneo hilo."
Ingawa serikali hiyo inawalazimisha wakaazi wa maeneo inayoyoyadhibiti kuhudumu katika jeshi, lakini inashaka na utiifu wao jambo linaloipelekea kuwategemea wanamgambo hao waliopigana katika upande wake wakati wa kipindi cha mapinduzi.

b. Kutegemea majeshi ya kieneo "ili kuweka amani", na

*Endelea Uk..15*



Email: info@uqab.or.ke

huenda ikavileta vikosi vya Misri, Saudi na Uturuki kwa lengo hili. Hizi si habari mpya; mtandao wa Al Jazeera Net ulinukuu gazeti la Amerika, 8/4/2016: “Gazeti la ‘American Journal’, maslahi ya kitaifa yanaelekeza katika vita ambavyo vimekuwa vikitokota nchini Syria kwa miaka, na kusema kuwa nchi hiyo imetumbukia ndani ya mgogoro unaohitaji vikosi vya kuweka amani, pasi na kutilia maanani ni muundo gani mzozo huo utakaomalizika kwao.” Dhana hii ya Amerika ya suluhusho nchini Syria inayotoa wito wa kusajiliwa kwa vikosi kutoka ng’ambo, licha ya mafanikio ya kijeshi ya Bashar, haijamalizika. Mtandao wa Al Jazeera Net ulinukuu mnamo 17/4/2018:

“Gazeti la Wall Street Journal liliripoti kwamba utawala wa Raisi Donald Trump unapanga kubadilisha vikosi vya Amerika kwa vikosi vya Kiarabu nchini Syria ili kudumisha ustawi katika eneo la kaskazini-mashariki mwa nchi hiyo baada ya ISIS kushindwa.

Gazeti hilo liliripoti kuwa mshauri wa usalama wa taifa wa Amerika John Bolton aliwasiliana na kaimu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Misri Abbas Kamil ili kujua msimamo wa Cairo kuhusiana na hili; liliongeza kuwa mawasiliano hayo yalifanyika pia kwa nchi za Ghuba, ili kushiriki katika majeshi haya na kutoa usaidizi wa kifedha kwayo. Maafisa katika utawala huo wanataraji kwamba nchi za Kiarabu zitajibu ombi hili la Trump, hususan katika usaidizi wa kifedha.)

8. Hili ndilo linaloashiriwa na ukweli uliojitokeza na unaojitokeza juu ya sera ya Amerika nchini Syria …

Na baada ya kufanya uchambuzi wake, ni wazi kuwa kuendelea kuwepo kwa serikali hiyo na wala sio kwa nini haikuanguka, kimsingi haitokamani na nguvu ya serikali hiyo au nguvu ya Amerika na wafuasi wake Urusi na Iran na wanamgambo wake, wala nguvu ya wafuasi na vibaraka wake Uturuki na Saudi Arabia, ingawa zinao ushawishi, bali sababu kuu ni khiyana au uhadaifu na ushirikiano wa viongozi wengi wa makundi katika kuiamini Amerika, kwamba iko pamoja nao, na kusahau kuwa yeye ni adui wa Uislamu na Waislamu katika matendo yake yote … pamoja na imani yao kwa wafuasi wa Amerika na vibaraka wao Uturuki na Saudi Arabia na kusahau kuwa Aleppo ilisalimishwa kupitia kufungua mpaka wa Ngao ya Furat na kuwaondoa wapiganaji huko, kisha ikaja Tawi la Zaituni iliyo waondoa wapiganaji huko, na kuiacha kusini mwa Idlib kuwa kitoweo rahisi cha Urusi na serikali.

Ama kuhusu Saudi Arabia, makundi yalisahau namna Saudi ilivyo yatayarisha kwa majadiliano na serikali ya katili katika mikutano na majadiliano yanayoitambua serikali hiyo zaidi kuliko kuing’oa. Na sasa Mfalme Mtarajiwa wa Saudi Arabia amefichua lile lililokuwa limefichika na kuweka wazi kuwa Bashar anabakia … na lililo baya zaidi ni kuwa Urusi inawalipua kwa ukatili huku wao wakijadiliana nayo na kusalimisha silaha zao nzito na wastani! Ni mandhari ya uchungu kuona kuwa Urusi inapokea vifaru vyao na bunduki zao, na wanakaribia kufedheheshwa na kudhalilishwa.

Yote haya ndiyo sababu msingi ya yanayo endelea. Wamedumu kwa miaka mingi katika mapigano na serikali na kuteka maeneo yake, lakini kwa siku chache tu waliiwacha Aleppo kwa kushirikiana na Uturuki. Walitoka eneo la kusini mwa Syria, hususan kutoka Daraa kwa siku chache zaidi, kwa kushirikiana na Saudi Arabia. Katika hali zote hizi, maghala yao ya silaha yalikuwa yamejaa silaha walizoziteka nyara kutoka kwa jeshi la serikali … Hakika inasikitisha kuwa wamevumilia miaka mingi ya ulipuliwaji kwa mabomu, makombora yenye maangamivu na silaha hatari kutoka kwa serikali, Urusi, Iran na wanamgambo wake, lakini wakapeana maeneo yao bila ya vita kwa siku chache, na kuyasalimisha kwa ushirikiano na khiyana, na hata kusalimisha silaha zao nzito na wastani! Na kuacha nyumba zao na kuwa wakimbizi!

Yeyote anayefuatilizia haya ataona kuwa sababu kuu ni uaminifu wa makundi haya kwa maadui wa Uislamu na Waislamu, na uaminifu wao kwa vibaraka na wafuasi, ima viogozi wa makundi hayo walijua hilo au la, ima walidhamiria hili au walifanya kwa makosa, yote haya ni uchungu … mtu anaweza kuuliza, na ana kila haki ya kufanya hivyo, maadamu Hizb ut Tahrir ina kiwango hiki cha utambuzi, maono na ufahamu na inayajua matukio, kwa nini haikuyashauri makundi haya na kuyapa utambuzi ili yasiingie katika makosa haya?

Mimi nasema kwa wale wanaouliza swali hili, kwamba sisi tumesheheni uchovu kwa kuwapa ushauri wetu kwao na kuwaonesha uhalisia wa mambo kwa dalili na uthibitisho … miguu yetu imechoka kwa kutembea kiguu na njia kwao ili kuwashauri na kuwaongoza, kwani baadhi ya njia zakuwafikia wao zilikuwa hazipitiki magari kwa urahisi. Kwa hivyo tulitembea kwa miguu, na kutokana na mawasiliano ya mara kwa mara nao, baadhi ya watu walidhani kuwa sisi ni miongoni mwao!!! Ikiwa mtu atasoma aliyeuliza swali hili atasoma matoleo yetu, na majibu ya maswali, na yako mengi mno, atajua kuwa tumetia juhudi nyingi juu ya jambo hili, zaidi kuliko uwezo wetu, lakini wengi wa viongozi hawa hawakumuitikia au kumuogopa (Allah), walikuwa wakisema, pindi tulipo waonya kuhusu kuchukua pesa chafu walizozichukua kutoka kwa nchi hizi za khiyana: “Tutapata wapi pesa kwengine? Hizb ut Tahrir haitupi pesa.”

Kwa hivyo wakajihalalishia kuchukua pesa kutoka kwa Makafiri na makhaini! Tukiwaambia kuwa mutakuwa mateka wao, wao husema hapana! Kwa hivyo kilicho potea kimepotea, wamebakia vipofu katika ujinga. Tukiwaambia kuwa mutapata silaha nyingi ambazo mutaziteka kutoka kwa serikali, sasa kwa nini basi mujifedheheshe milangoni mwa wale makhaini ili kupata baadhi ya silaha? Wao wanasema, tutapata wapi silaha zetu na Hizb ut Tahrir haitupi silaha? Tukiwaambia kuwa shingo zenu zitakuwa halali yao kwa silaha hizi, wao wanasema, tunachukua kutoka kwa adui na kupigana na adui! Hatimaye wakayaona haya, lakini ilikuwa washachelewa, kuwa walinyimwa silaha hizo walizokuwa na haja nazo sana, na hata kuzisalimisha silaha zao kwa njama za makhaini hao … Kwa hivyo tuliwashauri lakini hawakuwapenda washauri hawa! Kama mfano, nilitaja baadhi ya yale yaliyomo ndani ya toleo letu la mnamo 05/04/2018:

“… Ingawa chama kilitia juhudi kunyanyua utambuzi kwa makundi haya, na kuyaelimisha kuhusu yanayojiri, lakini yalikuwa yakihalalisha kuwafuata watu hao, kwa sababu walikuwa wakiwasaidia wao kwa pesa na silaha, na kwamba Hizb haiwezi kufanya hilo, bali inawasaidia kwa ushauri pekee … wanasema kuwa ushauri pekee hausaidii inapokuja katika vita kivitendo! Hawakutambua kuwa upanga mkononi mwa mwenye kuushika, una makali pande zote mbili, ni katika mkono wa mwenye utambuzi, aliye na maono, ngao inayomlinda kutokana na uovu wa hasimu wake, na mbinu zenye nguvu ya kumshinda adui yake … Lakini mkononi mwa aliyehadaiwa anayekimbia nyuma ya usaidizi wa wahalifu itakuwa ni ngao iliyo chanika, huku nyaya zikipenya katikati yake, na kumuua kila anayeibeba kabla ya kuuliwa na hasimu

*Endelea Uk..16*

wake!

Sisi tunayahutubia makundi hayo kuwa kukataa ushauri na utambuzi wetu, na kusema kuwa hausaidii wakati wa vita hivyo, na kwamba wanataka pesa na usaidizi wa silaha, wanaopata kutoka kwa makhaini wa Waislamu, Waarabu, Waturuki na Wafursi. Baadhi yao wakiongezea, hata kwa wahalifu wa Kirusi na wa Kiamerika, wakidhani kuwa kuchukua pesa hizo chafu kutoka kwao, hakutawazuia wao kutokana na kuipigania Ash-Sham … Tunawaambia wote hao: Sasa munajionea natija ya matendo yenu na maneno yenu, mumekuwa wakimbizi, muliofukuzwa majumbani mwenu na hata kwa watoto wenu!

9. Kwa kutamatisha, tunasema: hakuna hata eneo moja lililosalia isipokuwa Idlib, na pengine Erdogan ana ngao na matawi mengineyo yaliyoipoteza Idlib yatakayoipoteza Idlib na vitongoji vyake, ambayo iko kimya na haionyeshi harakati yoyote … Sisi tunayaambia makundi haya wasidanganywe na hatua za Erdogan na katu wasiisalimisha Idlib kwa serikali … Hawapaswi kuyasahau yale yaliyowatokea Aleppo, na kukumbuka Hadith ya Mtume (saw), iliyosimuliwa na Bukhari kutoka kwa Abu Hurayrah (ra) kwamba Mtume (saw) amesema:

**«لَا يُلْدَغُ الْمُؤْمِنُ مِنْ جُحْرٍ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ»**

"Muumini hang'atwi katika tundu moja mara mbili." Vipi basi ikiwa atang'atwa mara nyingi?

**﴿إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ﴾**

**"Hakika katika hilo upo ukumbusho kwa yeyote aliye na moyo au akatega sikio na yeye yupo anashuhudia (kwa kutafakari akili yake)"** [Qaf: 37]

Kwa kutamatisha, tunasisitiza yale ambayo tayari tushayasema: dhurufu zitabadilika, na Ummah huu umeathiriwa na hili na majanga mengine makubwa zaidi, mithili ya Makruseda ma Matartari, na hatimaye ukarudia tena izza yake na kuamka, na kuwang'oa na kisha kuuongoza ulimwengu … Ni kweli kuwa utawala wa Kiislamu ulitabikishwa siku hizo. Na kwamba Khilafah ilikuwepo hata ingawa ilikuwa dhaifu, Ummah ulikuwa na kiongozi aliye uunganisha kupigana na adui yake, kupata haki na kung'oa batili, ulimshinda adui yake na kuinuka tena. Leo hakuna utawala wa Kiislamu, hakuna Khilafah, na ruhusa kutoka kwa yule anaye waunganisha Waislamu kupigana, hili ndilo ambalo laweza kusemwa na mtu, na ambalo ndio wasifu wa kweli wa uhalisia, lakini kazi ya Khilafah inaendelea kwa nguvu, kwa idhini ya Allah, na imekuwa ndio matakwa ya Waislamu katika biladi zao, na wanatamani hili kwa maneno na vitendo, na wanazikabili siku zile nyeusi, 26, 27, 28 za Rajab 1342 H, zilizo husisha khiyana na uhalifu wa kuvunjwa kwa Khilafah, kuziondoa siku hizo nyeusi, na kurudisha tena Khilafah ili ing'are tena katika siku ambayo Allah (swt) ameikidhia. Hili ni rahisi kwa Allah (swt) kulitimiza. Hapo ndipo waovu, wale waliokhini, na madhalimu watakapojua mwisho wao utakuwa upi ...

Waislamu hawapaswi kukata tamaa na rehma ya Allah, Ash-Sham itabakia kuwa Ash-Sham, ndio nyumba ya Uislamu: Imesimuliwa na Na'eem Bin Hammad juu ya kadhia ya fitna, kutoka kwa Khatheer Bin Murrah: aliyesema:

Mtume (saw) amesema:
**«عُقْرُ دَارِ الْإِسْلَامِ بِالشَّامِ» "Kitovu cha nyumba ya Uislamu kiko Ash-Sham."**

Hizb imehakikishiwa tena kwa nusra ya Allah sio tu kwa Manabii na Mitume, bali pia kwa waumini, wakweli, na sio tu kesho Akhera, bali pia hapa duniani.

**﴿إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ﴾**

**"Hakika, Sisi kwa yakini tutawanusuru mitume Wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na Siku watakayosimama mashahidi."** [Ghafir: 51]

Na siku hiyo waumini watafurahi kwa nusra ya Allah, na waovu watadhalilika kwa fedheha na adhabu kali kesho Akhera, na Allah ndiye mlipaji kisasi (Muntaqim), Jabari, Mwenye nguvu (Aziz) na Mwenye hekima (Hakeem).

**16 Dhul Qi'dah 1439 H**
**29/7/2018 M**